



**Mhe. Ikupa asisitiza Itilima Kufanya ya fuatayo**

- **Kuharaki-sha mafunzo ya Vikundi vya watu Wenye ulemavu**
- **Lugha ya alama ipe-we kipaumbele kurahisisha mawasiriano kwa jamii ya watu wasiyo sikia**
- **Elimu ya CHF iliyo boreshwa iendelee kutolewa ili watu wawe na uhakika wa matibabu**

## MHE. IKUPA AIPONGEZA ITILIMA KWA KUENZISHA CHUO CHA MAFUNZO YA UFUNDI NA UJASIRIAMALI KWA JAMII YA WATU WENYE ULEMAVU



Naibu Waziri katika Ofisi ya Waziri Mkuu anaeshughulikia Watu Wenye Ulemavu Stella Ikupa Akiwa Kwenye Picha ya Pamoja Na Kaimu Mkuu wa Mkoa wa Simiyu Mhe. Festo Kiswaga wanne kutokea Kushoto na Kamati ya Ulinzi na Usalama ya Wilaya ya Itilima ikiongozwa na Mkuu wa Wilaya ya Itilima Mhe Benson Kilangi watatu Kushoto, Katibu Tawala wa Itilima Filbert Kanyirizu wa Pili Kulia Kaimu OCD kamanda Bwiru, watatu Kutokea Kushoto ni Mkurugenzi wa Halmashauri ya Itilima Bi. Elizabert Gumbo.

Naibu Waziri Katika Ofisi ya Waziri Mkuu ,Sera, Bunge, Kazi, Vijana, Ajira na Wenyeulemavu, Stella Ikupa ampongeza Mkuu wa Wilaya ya Itilima Mhe. Benson Kilangi na Wataalamu wa Halmashauri ya Wilaya ya Itilima kwa Kufungua Chuo cha Mafunzo ya Ujasiriamali na Ufundi kwa ajili ya Vijana, Wanawake na Watu Wenyeulemavu na Kiwanda cha Sabuni.

Akiwa katika kijiji cha Kanadi, Kata ya Chinamili, Wilayani Itilima Mhe. Ikupa alisema “ Mhe. Dc Nikupongeze kwa hatua ya kuwa na Taasisi ya Mfunzo kama hii, ni Mwanzo Mzuri na nimuhimu kwa Mustakabali wa Jamii ya Watu Wenyeulemavu na ikiwezekana Fursa hii ya Mafunzo itangazwe ili iwafikie wenye uhitaji kwa wingi Zaidi”

Aidha Mhe. Ikupa alitaka Halmashauri ya Itilima kupitia asilimia mbili ya Mapato yake iliyo tengwa kisheria kwa ajili ya watu wenyeulemavu, kuongeza kasi ya Kufikia Wahitaji wa Fursa za Mikopo kabla ya kipindi hiki cha bajeti kuisha.

Akiwa Wilayani Itilima Naibu Waziri huyo anayeshughulikia Watu wenye Ulemavu alipata fursa ya Kukutana na Jamii ya Watu wenye ulemavu na kujibu baadhi ya kero zao pia alipata fursa ya kukagua Mradi wa Kitalu Nyumba ambao siku chache zijazo utakamilika na utatoa mafunzo ya kilimo biashara kwa jamii kubwa ya vijana wa Wilaya ya Itilima.



Naibu Waziri Ikupa ikipewa Kasha la Sabu-na ya Kufulia ya WIZA inayo zalishwa ki-wandani hapo kutoka kwa Afisa Vijana wa Halmashauri ya Wilaya ya Itilima Nuru P. Kabawa.



Mhe. Ikupa akipokea maelezo ya jinsi ya utengenezaji wa Sabauni kutoka kwa mlezi wa Mafunzo wa Kiwanda cha Kuten-genezea Sabuni cha Kanadi



Mhe. Ikupa akisalimiana na Mbunge wa Jimbo la Itilima Mhe Njalu D. Silanga



Naibu Waziri anayeshughulika na watu wenye ulemavu Mhe. Ikupa akimsikiliza kijana mwenye ulemavu wa Kusikia aliyekua akitumia ludha ya ishara.